

# SHERIA ZA MBEGU NI NINI?

**S**heria za mbegu zinatungwa na serikali pamoja na tasnia ili kudhibiti sekta rasmi/biashara ya mbegu. Pia zinaweka viwango vya sekta ya biashara ya mbegu ndani ya nchi vinauyosimamia ubora na usafi wa aina za mbegu.

Sheria za mbegu zinajikita kwenye:

- 1 Mifumo mbalimbali ya utoaji wa aina za mbegu;
- 1 Uthibitishaji wa mbegu;
- 1 Taratibu za udhibiti wa ubora wa mbegu; na
- 1 Mifumo ya karantini na usafi – ili kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu.

Katika ngazi ya taifa, kuna kamati ya tolea ya aina za mbegu, taasisi za uthibitishaji wa mbegu na mifumo ambayo inafanya kazi kulingana na taratibu zinazohusiana na sheria za mbegu. Taratibu hizi zinafanya kazi kwa kupendelea makampuni binafsi ya mbegu yanayojihusisha na biashara ya mbegu zilizoboreshwa ili yaweze kutengeneza faida.

Ili mbegu ziidhinishwe kuuzwa katika nchi, lazima zifikie kigezo maalum, au kiwango, kinachoitwa DUS. (DUS inasimamia, *bainifu*, *inayofanana*, na *thabiti*.) Aina ya mbegu ambazo zitakuwa zimeidhinishwa zimeorodheshwa katika Orodha ya Aina ya Mbegu. Baada ya hapo, aina ya mbegu lazima zithibitishwe kulingana na kanuni na taratibu kali ambazo zinapima ubora na usafi wa mbegu.

Sheria ya Mbegu ni chombo kinachotumika kubadilisha na kudhoofisha mfumo wa mbegu unaosimamiwa na wakulima. Hii inaleta athari hasi kwenye uanuai na mifumo ya mbegu ya wakulima, na hata katika pato la familia na usalama wa chakula.

